

# Chanjo ya Watoto Wachanga

## Mwongozo kwa Wazazi

Hizi ndizo chanjo ambazo mtoto wako anahitaji!

Wakati wa kuzaliwa <sup>1,2</sup>	HepB	RSV-mAb <sup>1</sup> miezi 0-7									
Miezi 2 <sup>1,2</sup>	HepB miezi 1-2 <sup>2</sup>	+	DTaP	+	PCV	+	Hib	+	Polio	+	RV
Miezi 4 <sup>1,2</sup>	HepB <sup>3</sup>	+	DTaP	+	PCV	+	Hib	+	Polio	+	RV
Miezi 6 <sup>1,2</sup>	HepB miezi 6-18 <sup>2</sup>	+	DTaP	+	PCV	+	Hib <sup>4</sup>	+	Polio miezi 6-18 <sup>2</sup>	+	RV <sup>5</sup> + Mafua <sup>6</sup> + COVID <sup>7</sup>
Miezi 12 na zaidi <sup>1,2</sup>	MMR miezi 12-15 <sup>2</sup>	+	DTaP miezi 15-18 <sup>2</sup>	+	PCV miezi 12-15 <sup>2</sup>	+	Hib miezi 6-18 <sup>2</sup>	+	Teteku- wanga miezi 12-15 <sup>2</sup>	+	HepA <sup>8</sup> miezi 12-23 <sup>2</sup> + Mafua <sup>6</sup>

Wasiliana na daktari au muuguzi wako ili kuhakikisha kuwa mtoto wako anapokea chanjo zote zilizoratibiwa. Mara nyingi chanjo huchanganywa ili kupunguza idadi ya sindano. Hakikisha unaomba kadi ya kumbukumbu ya tarehe za chanjo za mtoto wako; njoo na hii kwa kila ziara.

Hapa kunayo orodha ya magonjwa ambayo mtoto wako atalindwa dhidi yao:

**HepB:** hepatitis B, ugonjwa mbaya wa ini

**DTaP:** diphtheria, pepopunda (taya kukwama), na kifaduro

**PCV:** chanjo ya pneumococcal conjugate hulinda dhidi ya maambukizi makali ya damu, mapafu, na ubongo

**Hib:** Mafua ya *Haemophilus* aina ya b, maambukizi makali ya ubongo, koo, na damu

**Polio:** ugonjwa mbaya wa kupooza

**RSV:** virusi vya mfumo wa kupumua, maambukizi makali ya mapafu

**RV:** maambukizi ya rotavirus, ugonjwa mbaya wa kuhara

**Mafua:** maambukizi makali ya mapafu

**MMR:** surua, mumps, na rubela

**COVID-19:** ugonjwa mbaya na unaoambukiza sana

**HepA:** hepatitis A, ugonjwa mbaya wa ini

**Teteku-wanga:** pia huitwa varisela

### Vidokezo kwa chati hapo juu:

1. Kuanzia Oktoba hadi Machi, watoto wachanga wanaozaliwa hadi miezi 7 wanaweza kuhitaji kingamwili ya kuzuia RSV (RSV-mAb) ikiwa chanjo ya RSV haikupeanwa wakati wa ujauzito. Baadhi ya watoto wachanga wakubwa wenye umri wa miezi 8 hadi 19 wanaweza kuhitaji RSV-mAb wakati wa msimu wao wa pili wa RSV.
2. Hiki ndicho kiwango cha umri unaopaswa kupewa chanjo hii.
3. Mtoto wako huenda asihitaji dozi ya chanjo ya HepB akiwa na umri wa miezi 4, kulingana na chanjo iliyotumiwa. Wasiliana na daktari wako au muuguzi.
4. Mtoto wako huenda asihitaji dozi ya chanjo ya Hib akiwa na umri wa miezi 6, kulingana na chanjo iliyotumiwa. Wasiliana na daktari wako au muuguzi.
5. Mtoto wako huenda asihitaji dozi ya chanjo ya RV akiwa na umri wa miezi 6, kulingana na chanjo iliyotumiwa. Wasiliana na daktari wako au muuguzi.
6. Watoto wote wenye umri wa miezi 6 na zaidi wanapaswa kupewa chanjo dhidi ya Mafua katika msimu wa mvua au wa masika wa kila mwaka.
7. Mtoto wako atahitaji dozi 2 au 3, kulingana na chanjo ya COVID-19 anayopewa.
8. Mtoto wako atahitaji dozi 2 za chanjo ya HepA, akipewa angalau miezi 6 moja baada ya nyingine.

Swahili translation provided by Fargo Cass Public Health

